KWAYA YA MTAKATIFU KIZITO
PAROKIA YA MWENYEHERI ANUARITE MAKUBURI
+255742000089|+255713975788
kmkmakuburi
www.kmkmakuburi.co.tz
stkizitochoir@gmail.com

EE MUNGU UNIREHEMU- V.MABULA

Utangulizi

Ee Mungu unirehemu sawa sawa na fadhili zako, kiasi cha wingi wa rehema zako uyafute makosa yangu, unioshe kabisa na uovu wangu

Kiitikio

Uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu, usinitenge na uso wako wala Roho wako Mtakatifu usiniondolee x2

Mashairi

1. Unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, unioshe nami nitakuwa mweupe, nitakuwa mweupe kuliko theluji unifanye kusikia furaha na shangwe.

2. Mifupa uliyoiponda ifurahi ifurahi, usitiri uso wako, usitazame dhambi zangu uzifute hatia zangu zote

3. Unirudishie furaha ya wokovu, unitegemeze kwa roho ya wepesi, nitawafundisha wakosaji njia, wakosaji njia zako na wenye upole watarejea kwako.